



Wizara ya Afya

Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma

Fomu ya Uchunguzi wa awali wa TB na Ukoma katika Jamii

Jina la Kituo: _____ Halmashauri: _____ Mkoa: _____

Fomu ya uchunguzi wa awali wa Kifua Kikuu na Ukoma: TB/LEP 12

Fomu hii inatumika kusajili wateja wote wanaopatiwa uchunguzi wa kifua kikuu (TB) na Ukoma kwenye jamii. Fomu hii inajazwa na mtoa huduma za afya ngazi ya jamii na ataitumia kila anapofanya zoezi la kuchunguza wateja wake kabla ya kuwapa rufaa ya kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Hakikisha sehemu zote zinajazwa ipasavyo

NAMNA YA UJAZAJI

Jina kamili la Mtoa huduma za afya ngazi ya jamii: Andika jina la mtoa huduma ngazi ya jamii wa eneo husika anae jaza fomu hii.

Jina la Kikundi/Asasi: Andika jina la kikundi au asasi inayo fadhili shughuli za TB/Ukoma katika eneo lako

Tarehe ya kutolea taarifa: Andika tareha ya kutolea taarifa ya mwezi husika kwa kufuata mtiririko wa siku/mwezi/mwaka (dd/mm/yyyy).

Jina la kitongoji /Mtaa: Andika jina kamili la kitongoji taarifa zinapokusanyiwa

Kijiji: Andika jina kamili la kijiji taarifa zinapokusanyiwa

Kata: Andika jina kamili la Kata taarifa zinapokusanyiwa

Halmashauri: Andika jina kamili la Halmashauri taarifa zinapokusanyiwa

Safu ya (1) Namba(serial): Andika namba mtiririko ukianzia na namba 1 na kuendelea kila mwanzo wa mwezi

Safu ya (2) Tarehe: Andika tarehe ambayo mteja alifanyiwa uchunguzi wa kifua kikuu au ukoma

Safu ya (3) Jina la mteja (Majina matatu): Andika majina matatu halisi ya mteja . (Herufi kubwa)

Safu ya (4) Jinsi (Me/Ke): Andika ME kama ni mwanamume, andika KE kama ni mwanamke.

Safu ya (5) Umri: Andika umri wa mteja kwa miaka kamili. Iwapo mteja ana umri chini ya mwaka mmoja andika sifuri (0)

Safu ya (6) Namba ya simu ya mteja na mtu wa karibu: Andika namba ya simu ya mteja msitari wa juu na namba ya mtu wa karibu msitari wa chini.. Mtu wa karibu anaweza kuwa ndugu yake au mtu yoyote anaemwamini kama hana ndugu.

Safu ya (7) Mahali Mteja Anapoishi (Kitongoji/Kijiji/Mtaa): Andika kitongoji/Kijiji/Mtaa mteja anapoishi kwa sasa

Safu ya (8) Uchunguzi wa TB au ukoma: Andika 1 kama ni uchunguzi wa TB, andika 2 kama ni uchunguzi wa ukoma. Kama atafanyiwa uchunguzi wa magonjwa yote, andika mistari miwili kila uchunguzi wa ugonjwa na mstari wake

Safu ya (9) Aina ya mteja au Mahali mteja alipofanyiwa uchunguzi: Weka au andika namba ambapo mteja alipofanyiwa uchunguzi kama ni;

Safu (9) i. Anaishi kaya au karibu na mgonjwa wa TB au ukoma: Andika namba 1 kama ni **ndiyo** na andika 2 kama ni **hapana**

Safu (9) ii. Kundi maalum: Andika namba ya kundi husika ambako mteja ametoka, mfano 1 kama ni Mchimbaji(machimbo/migodi), 2 kama ni mfungwa/Afisa wa magereza, 3 kama ni PWUD na 4 kama ni Mvuvi(kambi za Wavuvi).

Safu (9) iii. Mkusanyiko wa watu/sehemu nyingine: Andika namba ya mkusanyiko husika ambako mteja ametoka; mfano 1 kama ni Duka la dawa, 2 kama ni Mganga wa jadi ,3 kama ni Sokioni na 4 kama ni Nyumba ya Ibada.

Safu ya (10) Matokeo ya mahojiano kuhusu TB: Weka alama ya vema (\checkmark) kwenye safu ya dalili alizonazo mteja kwa kufuatisha kielelezo *.

Safu ya (11) Matokeo ya mahojiano kuhusu Ukoma: Weka alama ya vema (\checkmark) kwenye safu ya dalili alizonazo mteja kwa kufuatisha kielelezo ***.

Safu ya (12) Aina ya rufaa: Andika namba ya aina rufaa/namna ambayo mteja amepewa kama ilivyoainishwa kwenye safu hiyo (1. Sampuli; 2. Mteja).

Safu ya (13) Sababu ya Rufaa: Andika namba ya sababu ya rufaa ambayo mteja amepewa kama ilivyoainishwa kwenye safu hii (1. Vipimo; 2. Tiba Kinga, 3. Changamoto za Jinsia na haki za binadamu zinazohusiana na huduma ya Kifua Kuu na Ukoma)

Safu ya (14) Jina la kituo cha huduma za afya rufaa ilikoenda: Andika jina la kituo cha kutolea huduma za afya alipopolekwa mteja/sampuli kufanyiwa uchunguzi

Safu ya (15) Amepima VVU: Andika “N” kama mteja amepima VVU, andika H kama mteja hajapima VVU.

Safu ya (16) Maoni/Maelezo ya ziada: Andika maoni au maelezo ya ziada juu ya mteja huyu. Usirudie taarifa ambazo tayari umejaza mwanzo.

